



Ile nyota ikawaongoza hadi horini Maria na Yusufu walimokaa na mtoto Yesu. Wakipiga magoti wakimwubudu, wale wasafiri walimpa Yesu zawadi za kupendeza za dhahabu na manukato.

19



Mungu akawapa wale wazee hadhari kuwa warudi nyumbani kisiri. Herodi alikasirika sana alipogundua haya.

20



Kwa hamu ya kumwagamiza Yesu, kiongozi huyu mwovu aliwaua watoto wote wachanga wa kiume kule Bethlehemu.

21



Lakini Herodi hangeweza kumwagamiza mwana wa Mungu! Walipohadhariwa kwa ndoto, Yusufu aliwachukua Maria na

Yesu penye usalama kule Misri.

22

Kuzaliwa kwake Yesu



Herodi alipoaga dunia, Yusufu akawatoa Maria na Yesu Misri. Wakaishi katika mji mdogo wa Nazareti iliyokuwa karibu na ziwa la Galili.

23

Kuzaliwa kwake Yesu
Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,
inapatikana katika
Matayo 1-2, Luka 1-2

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."
Zaburi 119:130

Kimeandikwa na Edward Hughes
Kimeorodheshwa na M. Maillot

Kimetafsiriwa na Grace Chepkoech
Imerekeshwa na E. Frischbutter; Sarah S.

Hadithi 36 baadhi ya 60

M1914.org

Bible for Children, PO Box 3, Winnipeg MB R3C 2G1 Canada

Leseni: Unahaki ya kunakili au kuchapisha hadithi hii. Mradi tu.

Mungu anajua kuwa tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Mshahara wa dhambi ni mauti.
Mungu anatumenda sana hadi akamtuma mwana wake, Yesu, aje afe msalabani na alipe mshahara ule wa dhambi. **Yesu alifufuka** na akarudi mbinguni! Sasa Mungu anaweza kusamehe dhambi zetu.
Kama unataka kuondoka kwa dhambi zako, mwambie Mungu haya: Mungu mpendwa, ninamini kuwa Yesu alikufa kwa ajili yangu na anishi tena. Tafadhali njoo maishani mwangu na usamehe dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya na niwe nawe milele. Nisaidie niishi kwako kama mtoto wako. Yohana 3:16
Soma bibilia na zungumza na Mungu kila siku!

Kiswahili Swahili



Hapo zamani, Mungu alituma malaika Gabrieli kwa mwanamali mdogo n a wa kupendeza aliyetwa Maria.



Akamwambia, "Wewe utazaa mwana na jina lake utamuita Yesu. Yeye ataitwa mwana wa aliye juu. Yeye atamiliki milele."

"Hii itakuaje?" binti Yule aliuliza akiwa ameshangaa. "Mimi sijaolewa na mwanamume yeyote." Malaika akamwambia Maria kuwa mtoto angetoka kwa Mungu. Mtoto Yule hangekuwa na baba wa kibinadamu.

3

Malaika pia akamweleza Maria kuwa jamaa yake Elisabeti alikuwa amepata mimba katika uzee wake.

4

Maria alikuwa amepanga kuolewa na Yusufu. Yusufu alisikia vibaya aliposikia kuwa Maria alikuwa mjamzito. Alidhania kuwa mwanamume mwingine alikuwa ndiye baba ya mtoto.

5

Katika ndoto, malaika wa Mungu alimwambia Yusufu ya kuwa huyu alikuwa mwana wa Mungu. Naye Yusufu alikuwa amsaidie Maria kumlelea Yesu.

6

Yusufu alimwamini na kumtii Mungu. Naye pia alitii amri za nchi yake. Kwasababu ya amri moja, Yusufu na Maria walisafiri kutoka kwao hadi Bethlehemu, ili kulipa ushuru.

7

Maria alikuwa tayari kumzaa mtoto. Lakini Yusufu hakuweza kupata nyumba ya kukaa. Nyumba zote zilikuwa zimejaa.

8

Mwishowe Yusufu aliweza kupata malazi horini. Hapo, mtoto Yesu akazaliwa. Mama yake akamlaza ndani ya hori la kulia la ng'ombe.

9

Karibu na hapo, wachungaji walikuwa wakiwachunga kondoo wao. Malaika wa Mungu akawatokea na kuwapa habari lile njema.

10

"Amezaliwa kwenu siku ya leo katika mji wa Daudi mwokozi, ndiye Kristo Bwana. Mtankuta mtoto amelala katika hori ya kulia ya ng'ombe."

11

Ghafa, malaika wengi wengine wanaong'aa wakatokea, wakimsifu Mungu wakisema, "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia."

12

Wachungaji wakaharakisha kuelekea horini. Baada ya kumwona mtoto walimweleza kila waliokutana nao kumhusu Yesu.

13

Muda wa siku arobaini baadaye, Yusufu na Maria walimleta Yesu wenywe hekalu kule Yerusalemu. Hapo, mwanamume aliyetwa Simioni alimtukua Mungu kwa sababu ya mtoto, naye Anna, mtumishi mwingine wa Mungu, akamshukuru Mungu.

14

Wote walifahamu kuwa Yesu alikuwa mwana wa Mungu, mwokozi aliyekuwa amehidiwa. Yusufu akawatoa ndege wawili kama sadaka.

15

Hii ilikuwa sadaka ambayo kulingana na amri ya Mungu watu masikini walipaswa kuleta walipokuwa wanamlelea Mungu mtoto aliyezaliwa.

16

Muda mfupi ulipopita, nyota ya kipekee iliwaongoza wazee watatu wenye hekima kutoka nchi ya Magharibi kuja Yerusalemu. "Yuko wapi Mfalme wa Wayahudi aliyezaliwa?" wakauliza. "Tunataka kumwuabudu."

17

Mfalme Herodi akasikia kuwahusu wale wazee wenye hekima. Akiwa na wasiwasi akawaambia wamueleze watakapompata Yesu. "Pia nami nataka kumwuabudu." Herodi akawaambia. Lakini alikuwa anawadanganya. Herodi alitaka kumwua Yesu.

18